



Utangulizi

Mtumishi wa Mungu: Eng John James Ndindwa

Subject: IBADA YA MEZA YA BWANA | 01.03.2020 AT BWC

Contact: Email: [ndindwajohn@gmail.com](mailto:ndindwajohn@gmail.com) | Cell: 0717 401 569 |

Luka 22: 17-20 Akapokea kikombe, akashukuru, akasema, Twaeni hiki, mgawanye ninyi kwa ninyi; Maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja. Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, **Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.** Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula; akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu.

## IBADA | KITENDO

Tukio la mwanadamu kumfanya Mungu maabudu. Kusali ni zile taratibu (michakato) mbali mbali zinazofanya maabudu yakamlike. *Namna ya kuomba, Namna ya kuendesha neno na mahubiri, namna ya kumsifu Mungu na kumwabudu Mungu.*

*Wakolosai 3:16 Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema miyoni mwenu.*

### Maabudu ni ya mwilini na rohoni.

*Warumi 12:1 Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.*

*Math 15:9 Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami.*

*Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu. Amos 5:23 Niondoleeni kelele za nyimbo zenu; kwa maana sitaki kuzisikia sauti za vinanda vyenu.*

Aina ya Maabudu | Ibada

- Yenye maana:** Rumi 12:1, Inahusisha watu walikubali kufa na kufufuka na kuwa familia na milki ya Mungu kwa njia ya Ubatizo wa Maji, Moto na RM. Maeneo mengine kama Mkristo hajafunga ndoa halali na mke ama wakabarikiwa baada ya kuweka agano kwa Mchungaji kwa niaba ya Mungu.

Si mtu wa dhambi tena.

*1 Wakorintho 11:27 Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.*

*Yohana 6:54 Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. 6:56 Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake.*

**2. Yasiyo na maana:** Math 15:9, Amos 5:23: Inahusisha makutaniko ya kidini yaani watu wanaomkuri Yesu kuwa ni Bwana kwa midomo yao huku mioyo yao iko mbali na Mungu.

Mkristo aliyewahi kuokoka na kuachana na dhambi kabisa akarudia kuwa mtu wa dhambi. Mtu aliyekufa katika mauti ya Yesu, akafufuka na kisha akarudia dunia. Ni sawa na mtu kutangaza kufa mara ya pili ambapo Kalvari ya Pili ya Yesu.

## MEZA YA BWANA

*Meza ya Bwana ni moja ya Maagizo makuu ya Bwana wetu Yesu Kristo kwa kanisa, pamoja na Ubatizo wa maji haya ni maagizo makuu pamoja na kuhubiri injili. Kutokana na maagizo haya moja ya mambo ambayo Yesu alituagiza tumkumbuke kwa mateso yake ni kwa njia ya kula mwili wake na kuinywa Damu yake kama kumbukumbu ya mateso yake.*

### Maana ya meza ya Bwana

1. Ni mojwapo ya agizo kuu la Bwana mwenyewe kwa mitume na Kanisa lake, Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. 1Wakortho 11:25

Neno “*Meza ya Bwana*” huitwa pia “*chakula cha Bwana*” ni ushirika wa kiroho kwa kushiriki **mwili** na **damu** ya Yesu. Hivyo ni njia ya kipekee ya kukumbuka agano alilofanya Mungu kwa ajili ya waamini wenye kushiriki meza ya Bwana.

2. Ni kumbu kumbu ya agano alilofanya Mungu na waumini wake (Kushiriki meza ya Bwana) ibada ya ushirika mtakatifu.

Hakuna njia ya mkato ya kumkumbuka Yesu hakutuagiza kuweka sanamu au chochote mfano wa mbinguni *bali kula na kunywa damu na mwili wake tu, Fanyeni hivi kwa ukumbushio wangu.....Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa, Kikombe akisema, kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. 1Wakortho 11:25*

3. Meza ya Bwana ni kielelezo au ishara kwamba waamini wanakuwa na ushirika mzuri na Bwana Yesu. Kupitia mwili na damu yake Yesu, tunafanywa imara imani zetu tukiamini kwamba ushirika huu tutakuwa nao pia kwenye karamu ya mwisho huko mbinguni (Ufunuo 19:9).

*Tukitazamia karamu ya arusi huko mbinguni (Ufunuo 19:9), inatusogeza pamoja na kutuimarishe imani zetu kwamba tunaamini tutakutana na mwanakondoo wa Mungu huko mbinguni katika arusi moja*

## MAJINA YA MEZA YA BWANA

Meza ya Bwana hutambulika kwa majina kadhaa kama ilivyoelezwa kwenye maandiko matakatifu.

- Meza ya Bwana (Lord's Table)

- Ushirika Mtakatifu (Holy Communion)
- Chakula cha mwisho (Last Supper)

## **ILIANZISHWAJE?**

*Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. 1Wakortho 11:25*

*Mat 26:26-29, Nao walipokuwa wakila, alitwaa kate, akabariki, akaumega, akawapa, akase ma, Twaeni ;huu ndiyo mwili wangu...*

Hivi leo Tunapokula Meza ya BWANA, Tunakumbuka “***pasaka***” kama jina la mwanakondoo aliyechinjwa kwa ajili ya ukombozi kwa sababu meza ya Bwana inahusisha mwili na damu ya Yesu. Tunafahamu ya kwamba wana wa Israeli walikuwa utumwani Misri muda wa miaka mia nne na thelathini /430 (Kutoka 12:40). Bwana Mungu alihitaji damu ya kondoo (pasaka) ipakwe kwenye miimo ya milango katika nyumba za wa-Israeli, kisha Bwana atapita juu yao yaani “ *ata-pass over*“. Kwa maana ndio asili ya neno “***pasaka***” (Kutoka12:13).

Siku ya kutoka kwa wana-Israeli utumwani Misri, ilikuwa ni siku kuu na Bwana akawaambia **waikumbuke siku kuu hii katika amri ya milele(Kutoka 12:14)**. Kwa kuwa sikukuu hii ni ya kukumbukwa milele, basi hata wazee wa Yesu (Mariamu na Yusufu) walikuwa wakienda Yerusalem kila mwaka wakati wa sikukuu ya pasaka, Yesu naye akaenda nao ( Luka 2:41-42)

## **WHY MKATE NA DIVAI**

“kama vile mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja.” Mkate mmoja uliovunjwa vunjwa kuliwa na wote, Yesu kusulibiwa kwa ajili ya wote, Damu yake kwa ajili ya wote. Wote walinywea kikombe kikombe.

*“Zamani vijijini tulikuwa tunakula ubwabwa sinia moja, Ugali mmoja na Mboga kwenye bakuli moja, ndio mana Upendo wa watu wa kijijini hauna choyo wala ubinafsi. Lakini mjini tangu imeanza self service wanahofia Budget watu wa mjini, Utasikia ukitaka kuja kunitembelea utoe taarifa na ikiwezekana uje na kifurushi cha mchele ili usione aibu ukitembelea ndugu wa dar. Watu wa kijijini hawahofii maisha kwa sababu ya chakula, watu wa mjini wanahofia maisha kwa sababu ya chakula.*

*Luka 22:19 Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*

*Yohana 6:54, 56 Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani*

yake. Yohana 15:4 Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu.

### **Whay mkate? Na tafsiri ya Bethlehemu**

#### **Kwa nini mkate na divai inatumika?**

1. Mkate hutumika kama mwili wa Yesu ( 1 Wakorintho 11:24)
2. Divai hutumika kama damu ya Yesu ( 1 Wakorintho 11:25)

Mika 5:2 Bali wewe, **Bethlehemu Efrata, (Mji wa Chakula Kiitwacho Mikate)** uliye mdogo kuwa mionganini mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli (**Yesu**); ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele (*Jesus was God on earth who existed forever*). Yesu alizaliwa Bethelemu ya uyahudi (*Mji wa Daudi,*)

**Yesu alizaliwa mji wa Mikate:** Yeye mwenyewe ndiye mkate kama chakula cha uzima, Yoh 6:54

**Mkate ulioshuka toka mbinguni:** Yesu ni Mkate ulioshuka toka mbinguni kuwa chakula cha wote.

1. **MANA ILISHUKA TOKA MBINGUNI ENZI ZA MUSA – AK** (Ukombozi wa Israel toka nchi ya utumwa na si toka dhambini na waliila miaka 40 pekee

Musa alikuwa ni mtoto wa 4 wa Lawi (Yokebedi) alikuwa Misri akamzaa Musa. Lawi lilikuwa ni Kabilia ambalo halikupewa urithi wa ardhi enzi Joshua kanani kwa kuwa sehemu yao ilikuwa ni **Hekaluni pekee.**

2. **NENO ALISHUKA KWA JINA LA YESU – AJ** (Ukombozi wa wanadamu wote) Neno hana mwanzo wala mwisho.

**Yohana 1:14** Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaan neema na kweli.

**Yohana 6:51,54** Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka **kutoka mbinguni;** mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu. Aulaye **mwili wangu** na kuinywa damu yangu anao **uzima wa milele;** nami nitamfufua siku ya mwisho.

-Mkate ulioshuka kutoka mbinguni uliitwa Mana ambao walikula miaka 40 Kuelekea kanani. Mkate ulioshuka kwa Jina la Yesu unahu su watu kuishi milele na kuelekea uzimani.

### **RADHA YA MKATE**

Kutoka 16:31 Na nyumba ya Israeli wakakiita jina lake **MANA;** nacho kilikuwa mfano wa chembe za mtama, nyeupe; na tamu yake ilikuwa kama **tamu** ya maandazi membamba yaliyoandalialiwa kwa asali.

Ezekieli 3:3 Akaniambia, Mwanadamu, lisha tumbo lako, ulijaze tumbo lako kwa hili **gombo nikupalo.** Ndipo nikalila, nalo kinywani mwangu **lilikuwa tamu**, kama utamu wa asali.

**CHAKULA CHAKE** – kinachochakatwa kwenye Kiwanda cha Kusafisha **Dhambi** kwa wanadamu ili kujitengeneza Taifa la Mungu la kanisa la wazaliwa wa kwanza.

1. **Maji** = Uzima
2. **Damu** = Uhai      Yesu alikuja kutengeneza Sin Cleaning System (Factory) katika chumba maalumu cha Usafi.
3. **Nyama** = Protein | Kujenga
4. **Ngozi** = Ulinzi | Mith 4:23

## **FAIDA ZA KUSHIRIKI MEZA YA BWANA**

1. Tunapata ushirika kamili na Kristo kupitia kikombe cha Damu yake na mkate amba ni mwili wake.
2. Basi Yesu akawaambia,Amini amini, nawaamba ,Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake,hamna uzima ndani yenu.Yohana 6:53.
3. Katika ushirika wa meza ya Bwana tunapata uzima wa milele na tunakaa ndani ya agano la damu na mwiliwake Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu ,nami hukaa ndani yake. Yohana 6:56
4. Tunapata uhai na uzima katika miili yetu, Uponyaji na nguvu za ki-ungu kupitia damu ya Yesu. Yohana 6:57-58, Kama vile Baba aliye hai alivyonitura mimi,nami ni hai kwa Baba,kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi. Hiki ndicho chakula kishukacho kutoka mbinguni; si kama mababa walivyokula, wakafa; bali akilaye chakula hicho ataishi.

Note: Kwa kuwa wana wa Israeli waliokolewa na damu ya mwanakondoo aliyechinjwa kwa aliji yao,vivyo hivyo nasi tunaokolewa na damu ya mwanakondoo wa Mungu aliye hai hata sasa,ambaye ni Bwana Yesu. Yesu Kristo pia ni pasaka wetu “*Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo;*”

Ikumbukwe: 1 Wakorintho 5:7. Kumbuka; meza ya Bwana sio pasaka,bali ni ushirika wa mwili na damu ya Yesu. Mausiano ya mwili na damu ya Yesu ndio yamegusia pasaka na ukombozi wa watu wa Mungu waliokuwa utumwani.

## **Mifano katika biblia**

1. *Kwenye hema ya kukutania ( Walawi 24:5-9)*
2. *Karamu ya pasaka ya kwanza ( Kutoka 12:13-28)*

3. Karamu ya mwisho ya Yesu (Luka 22:14-23)
4. Baada ya ufufuko wa Yesu (Luka 24:30,41-43, Yoh.21:9-14)

### Faida | Hasara ya kushiriki meza ya Bwana

1. Tunapata ushirika kamili na Kristo kupitia kikombe cha Damu yake na mkate amba ni mwili wake.
2. Basi Yesu akawaambia,Amini amini, nawaamba ,Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake,hamna uzima ndani yenu.Yohana 6:53.
3. Katika ushirika wa meza ya Bwana tunapata uzima wa milele na tunakaa ndani ya agano la damu na mwiliwake Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu ,nami hukaa ndani yake. Yohana 6:56
4. Tunapata uhai na uzima katika miili yetu, Uponyaji na nguvu za ki-ungu kupitia damu ya Yesu. Yohana 6:57-58, Kama vile Baba aliye hai alivyonitura mimi,nami ni hai kwa Baba,kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi. Hiki ndicho chakula kishukacho kutoka mbinguni; si kama mababa walivyokula, wakafa; bali akilaye chakula hicho ataishi.
5. Kuleta uponyaji. Kumbuka kwamba; Damu ya Yesu imetukomboa,imetuponya ( Isaya 53:4-5). Tunapotumia damu ya Yesu leo,tunaleta uzima ndani yetu na kuondosha mauti,magonjwa. Damu ni uhai ( Walawi 17:11)
6. Kitendo cha kuinywa damu ya Yesu na kuula mwili wake ni kitendo cha kukaa ndani yake naye kukaa ndani yetu (Yoh.6:56)
7. Kuleta ushirika kati yetu na Yesu.Kumbuka hili ni agizo tuliloagizwa kwamba “...fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu” Luka 22:19

### MAANA YA KUJIHOJI | VIGEZO VYA KUSHIRIKI

Yafaa kila mmoja wetu ashiriki meza ya Bwana kwa maana Bwana Mungu hajatenga na kubagua watu,bali Yeye Mungu anapenda kwamba kila mwamini aweze kushiriki meza ya Bwana, lakini sasa,imekuwa ni vigumu kushiriki sote kwa maana si wote wenye vigezo.

Ninapozungumzia neno “**vigezo**” lina maana ya usafi wa kiroho wa mwamini anayetaka kushiriki. Je hali yake ya usafi wa kiroho ikoje?

Hivyo basi anayestahili kushiriki meza ya Bwana ni **mwamini wa Kristo**,aliyesamehewa dhambi na kwa wale wasioamini hawapaswi kushiriki (1Wakorintho 10:21).

Kwa sababu Kila mwamini anapaswa afanye toba kabla ya kutumia meza ya Bwana. Biblia inasema;“ *Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.*” 1 Wakorintho 11:28.

Ni lazima kila mwamini ajihoji,neno “*ajihoji*” maana yake-mtu ajiangalie,mtu ajichunguze kwanza. Mtu ambaye amejichunguza na kujiona ana hatia ndani yake ni vyema asitumie meza ya Bwana kwa sababu waweza kupata laana badala ya baraka.

*Wafilipi 4:8 Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.*

Anayeshiriki ni lazima awe ameokoka na kuwa na mahusiano mazuri na Mungu. Kwa kuwa meza ya Bwana ni ibada ya kushiriki mwili na damu ya Yesu, basi kila mwamini anapaswa atubie dhambi zake zote. Hakuna hasara ikiwa kama watashiriki wachache wasiokuwa na vipingamizi.

### Tito 2:11-13

*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi (*Uhai*) yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudhi katika matendo mema.*